
# LUGHA NA FASIHI
## katika Mshikamano wa Kitaifa na Uwiano
## Barani Afrika




WAHARIRI

John Kobia
Mosol Kandagor
Leonard Chacha Mwita

# SURA YA KWANZA

## Fasihi ya Watoto kama Njia ya Kukuza Mshikamano wa Kitaifa

Pamela M. Y. Ngugi
*Chuo Kikuu cha Kenyatta*

**Utangulizi**

Lengo la nchi yoyote iliyojikomboa kutokana na ukoloni na kupata uhuru ni kugeuza asasi za kiukoloni ilizorithi ili ziweze kuhudumia mahitaji na tamaduni za jamii mpya (Ochieng, 1985 katika Mbatia, 2012). Kenya ilipopata uhuru mwaka wa 1963, na kikwazo kikuu katika ujenzi wa taifa jipya kilikuwa ni ukabila. Wakenya waliendelea kudumisha uaminifu kwa makabila yao kama ilivyokuwa kabla ya ukoloni. Hivyo basi kulikuwa na haja ya kubuni njia za kukabiliana na hali hii. Ujenzi wa utambulisho wa kitaifa ni muhimu katika kupunguza migogoro ya kikabila na kimbari. Utambulisho huu hauji kisadfa bali hujengwa kimakusudi kama sehemu ya ajenda ya viongozi wenye mtazamo mpana na urazini wa kitaifa. Kama anavyosisitiza Njogu (2012) "Utambulisho wa kitaifa unasaidia katika kuimarisha asasi za utawala bora, kuwajibisha viongozi na kuweka uwazi katika utoaji huduma kwa umma." Tangu enzi za kabla ya uhuru hadi sasa, Kiswahili kama lingua franka kimeweza kutoa mchango muhimu katika kujenga mshikamano wa kitaifa, (Mbatia, 2012). Kwa mfano, mara tu baada ya uhuru Kiswahili kilichangia katika kujenga tabaka la wafanyikazi ambalo lilijumlisha watu kutoka makabila mbalimbali. Watu waliotoka mashambani na kuja kufanya kazi katika miji mbalimbali walilazimika kutumia Kiswahili ili kuweza kuwasiliana. Hivyo basi lugha ya Kiswahili ikawa mojawapo wa nyenzo za kujenga utaifa wa Kenya.

Baada ya uhuru, serikali ya Kenya iliteua Tume ya Ominde chini ya Uenyekiti wa Prof. S.H. Ominde. Jukumu la tume hiyo lilikuwa ni kushauri serikali kuhusu utungaji na utekelezaji wa sera ya elimu baada ya kufanya uchunguzi uliohitajika. Tume hii iliibuka na malengo kadhaa ya elimu nchini Kenya.Lengo mojawapo la elimu lilikuwa na lingali ni kukuza utaifa, uzalendo na kuendeleza umoja wa taifa. Hivyo basi, elimu inayotolewa inahitaji kuziheshimu tamaduni mbalimbali zilizopo nchini na wakati uo huo, kuhakikisha kuwa haiendelezi ubaguzi katika jamii kwa misingi ya rangi, ukabila na dini. Ili kutekeleza lengo hili na malengo mengine, wasomi wengi wanaamini kuwa ufundishaji wa fasihi kwa jumla na hasa fasihi ya watoto unaweza kuchangia katika kuyafikia malengo haya kwa kukuza hisia za kitaifa miongoni mwa wanafunzi.

Ujenzi wa taifa ni juhudi za makusudi na za kujitolea. Tangu uhuru, wananchi wamekuwa wakitafuta njia za kuleta utangamano baina ya makabila na nchi mbalimbali za Afrika. Hatua moja kuhusu ujenzi wa taifa ni uimarishaji wa utamaduni wa tamaduni mbalimbali. Utamaduni wowote ule utaeleweka vyema kwa kuchunguza mila na desturi zilipo katika jamii husika, pamoja na kufahamu namna kila jamii ilivyowasilisha amali zake mbalimbali kama vile, ukarimu, kujitolea, haki na maslahi ya pamoja, mambo ambayo yalichangia katika kuunda utaifa. Ufahamu wa amali hizi waweza kupatikana kupitia fasihi za jamii hizi. Fasihi ni matokeo ya shughuli za jamii; huibuka, hukua na kusambaa kutokana na mazingira yaliyopo katika jamii. Lengo la sura hii ni kubainisha dhima ya fasihi ya watoto kama kichochezi cha kujenga

mshikamano wa kitaifa sawia na mshikamano wa eneo la Afrika Mashariki na Bara la Afrika kwa ujumla.

**Dhana za Taifa na Utaifa**

Kabla ya kushughulikia suala la jinsi fasihi ya watoto inaweza kutumiwa kuwafunza watoto utaifa na utangamano wa kijamii, ni muhimu kutambua kwanza dhana mbili muhimu ambazo zinahusika na utaifa nazo ni; taifa na utaifa.

**Dhana ya Taifa**

Taifa ni kikundi kikubwa cha watu ambao wameunganishwa na historia moja, wana kizazi kimoja, tajriba sawa, lugha moja na utamaduni mmoja. Kutokana na maelezo haya kuna uwezakano kwamba taifa linaweza kuvuka mipaka na kujipata katika nchi jirani. Aidha, linaweza kudumu bila hata kuwa na mipaka wazi ya kijiografia au serikali rasmi (Ngugi, 2012). Dhana ya taifa inaweza kueleweka vizuri hasa tukiifananisha na dhana ya taifa-finyu. Taifa-finyu ni dhana inayorejelea kikundi cha watu wanaohusiana kwa lugha, mila, desturi na utamaduni; ni kama familia moja kubwa. Dhana ya taifa-pana na taifa-finyu zinaingiliana ila kwamba dhana ya taifa-pana huwa na kipengele cha kisiasa nayo dhana ya taifa -finyu hurejelea kitambulisho cha kijamii na kiuchumi. Dhana ya taifa pana ina asili yake kutoka nchi za Ulaya kwani mipaka ya mataifa kama ilivyo leo ilichorwa na wakoloni bila kuzingatia makabila yaliyokuwemo, utamaduni wa watu na misingi ya kiuchumi ya makabila husika. Hali hii ilitokea baada ya Kongamano la Berlin la 1885, lililogawa mataifa ya Afrika katika nchi tunazozijua sasa. Tukichukuwa fasiri hizi, tunapata kuwa nchini Kenya kuna mataifa-finyu mengi. Kila taifa-finyu lina lugha, mila, desturi na tamaduni zinazoitofautisha na taifa-finyu lingine. Kwa ujumla, nchi ya Kenya inakuwa ndiyo taifa-pana linalobeba mataifa-finyu takribani arobaini.

Kijelezi cha taifa-finyu kimetumika hapa badala ya kabila kutokana na mwelekeo hasi ambao umekuja kuhusishwa na dhana ya ukabila. Neno ukabila lilitumika nyakati za ukoloni kama njia ya kumtenga Mwafrika na mzungu kwa maana ya mtu mjinga, mpumbavu na asiyestaraabika. Kwa sasa linatumika kama njia moja ya kuwagawa Wakenya katika makundi mbalimbali ambayo pia yanazua mwelekeo hasi miongoni mwa Wakenya wenyewe.

**Dhana ya Utaifa**

Utaifa huelezeka kama harakati ambapo wananchi hukuza na kuendeleza utambuzi wa kuwa wao ni sehemu ya nchi fulani; hivyo basi, nchi hiyo ni urithi wao. Huwa kuna hali ya kujivunia nchi katika kuwa mmoja wa taifa husika (The Constitution of Kenya Review Commission, 2001). Dhana ya nchi inatumika hapa kama taasisi iliyoundwa na wanajamii ambao wanamiliki sehemu fulani ya kijiografia kwa lengo sawia na wako chini ya serikali moja. Utaifa huibuka pale ambapo wananchi huwa wamefikia kiwango cha juu cha umoja kijamii na kisiasa. Hii ina maana kwamba idadi yote ya watu iweze kuhisi kwamba kuna umoja au wameunganishwa pamoja na amali au maadili fulani ya pamoja au kaida fulani za pamoja.

Pale ambapo nchi inajumlisha mataifa-finyu mbalimbali kama ilivyo nchini ya Kenya, makundi haya ya mataifa-finyu yanaweza kuunda taifa-pana. Hali hii inaweza kutokea iwapo wanaweza kuwa na umoja na utamaduni sawia kando na tamaduni zao za mataifa-finyu. Harakati ya kuendeleza umoja huu ndio inayojulikana kama ujenzi wa taifa-pana na matokeo ya harakati ya ujenzi wa taifa-pana ndio hujulikana kama utaifa (The Constitution of Kenya Review Commission, 2001). Dhana hii ya ujenzi wa taifa-pana vilevile hurejelea ile hali ya kuchangia katika kuboresha taifa-pana kwa kushiriki katika miradi ya ujenzi wa taifa. Hivyo, kuchangia

katika harakati za kidemokrasia na vilevile kuchangia katika miradi ya maendeleo ni namna ya ujenzi wa taifa.

Taifa huwa na vipengele ambavyo huvitofautisha na mataifa mengine. Baadhi ya vipengele hivi ni pamoja na; mipaka ya nchi, historia moja,malighafi ya pamoja,Jumla ya idadi ya watu,lugha Moja naishara za kitaifa, sikukuu za kitaifa na uhuru wa nchi. Mipaka ya nchi hulindwa na jeshi ili taifa lisivamiwe na majambazi. Hata ingawa nchi ya Kenya ina mataifa-finyu mengi na historia tofautitofauti, mataifa haya yanaweza kuwa na tajriba moja ya kihistoria. Kwa mfano, tajriba za enzi ya ukoloni na harakati za kupigania uhuru ni namna moja ambayo ilizua historia moja ya nchi na ikaleta utaifa.Mito, maziwa, misitu, madini, wanyama na mimea ni malighafi inayochochea kujivunia nchi na kuwapelekea wananchi kutaka kulinda na kutunza malighafi zao kwa manufaa yao na ya vizazi vijavyo.Utaifa hujumlisha miundo ya kitaifa na vilevile ishara ambazo huwaleta watu pamoja hata ingawa wana tofauti zao kijamii au kiuchumi na hata kisiasa. Jumla ya idadi ya watu ni malighafi ya nchi. Kuwa na idadi huweza kuamsha hisia za kujivunia nchi.Lugha moja huweza kuendeleza na kuimarisha utaifa hasa inapotumika kama kivuko cha mataifa-finyu mbalimbali na hata tamaduni tofauti. Lugha hii yaweza kutumiwa kuunganisha mataifa yote katika nchi. Jambo hili huzidisha kitambulisho cha utaifa na kujivunia nchi.Ishara za kitaifa huwa ni vyombo kama vile bendera, nyimbo za kitaifa na hela za nchi. Uhuru wa nchi ni kipengele muhimu kwa sababu nchi iliyotawaliwa na nchi nyingine haiwezi kuwa taifa.

Kinyume na vipengele hivi, utaifa uliojengeka katika misingi ya kikabila huwa na lengo la kutetea na kuhifadhi utamaduni wa kabila na mara nyingi hutumia uwezo wao wa idadi au wa kiuchumi kuishinikiza serikali husika kuchukua hatua au mwelekeo fulani ( Njogu, 2012). Kwa mujibu wa Mbatia (2012) nguzo muhimu ya utaifa ni utamduni wa kitaifa. Hivyo basi, hatua mojawapo katika ujenzi wa taifa ni uimarishaji wa utamduni wa kitaifa. Msingi na chombo cha kupasha utamuduni huu ni lugha. Lugha ya pamoja ndiyo inayozaa vipengele vya utamaduni kama vile fasihi na muziki. Kupitia lugha, wanajamii hujieleza na hufinyanga maisha yao na historia yao kupitia sanaa na simulizi za aina mbalimbali. Kwa jumla, lugha kupitia fasihi hutuwezesha kujifahamu sisi ni kina nani, tumetoka wapi na tunatarajia kwenda wapi.

Fasihi ni matokeo ya shughuli za kijamii; huibuka, hukua na kusambaa kutokana na mazingira yaliyoizunguka jamii husika. Kwa sababu hiyo kupitia kwayo, fasihi husterehesha na pia inafundisha maadili na mbinu za kuishi katika jamii. Fasihi hivyo basi ni falsafa ya maisha ya binadamu. Fasihi husimulia au kueleza hali na matukio katika jamii fulani maalum. Usimulizi huo unaweza kuhusiana na matukio halisi au ya kufikirika tu. Kwa kuwa fasihi hudhihirisha utamaduni wa jamii, basi inaweza kuelezwa kama ni nembo ya jamii (Simala, 2006). Vile vile, fashi ni ithibati ya maisha ya jamii inayosimuliwa kwa namna mbalimbali. Masimulizi haya hudhihirika kupitia fasihi andishi au simulizi ambazo hubainika kupitia fani kama vile methali, vitendawili, nyimbo, misemo, visaali, hadithi za kihistoria na za kihalisia. Tanzu mbalimbali za fasihi zina uhusiano wa kuwa na dhima ya kueleza, kuendeleza na kuhifadhi utamaduni wa jamii.

Kwa muda mrefu nchi ya Kenya imeshuhudia kuwepo kwa uhasama baina ya makabila mbalimbali hai ambayo imezua shaka na maswali mengi kuhusu hai ya utaifa na utangamano wa nchi. Hali hii imewaathiri watoto kwa viwango mbalimbali hivi kwamba hata watoto wanaingizwa katika swala la ukabila, jambo ambalo hapo awali hawakulifikiria. Watoto wamejipata na maswali mbalimbali ambayo hawawezi kuyajibu. Matokeo ya hali kama hii ni kwamba watoto wanaweza kukosa imani katika taifa lao. Makala hii inalenga kuangazia fasihi ya watoto na jinsi fasihi hii inavyoweza kutumiwa katika ujenzi wa taifa na utaifa miongoni mwa watoto. Hii inatokana na sababu kuwa watoto na swala zima la utoto ni muhimu katika mjadala

mzima wa elimu na utaifa. Ni muhimu kuwajali watoto kwa sababu bila watoto, kesho ya hivi karibuni haitakuwepo. Kwa hakika fasihi inaweza kutumia vema kama kichochezi cha kuwaelimisha watoto kuhusu masuala za utaifa, umoja na utangamano.

**Dhana na Dhima ya Fasihi ya Watoto**

Fasihi ya watoto ni fasihi iliyoandikwa kwa minajili ya kusomwa na watoto. Hii haimanishi kuwa fasihi hii haiwezi kusomwa na watu wazima. Fasihi ya watoto huwa imeandikwa kwa kuzingatia msomaji ambaye hasa tajriba yake ya maisha ingali finyu na vilevile uelewa wake wa mambo ungali unakua. Hivyo basi, fasihi hii huwalenga watoto kutokana na hali kwamba wao ni binadamu ambao wanaendelea kukua kiakili, kilugha na kimaumbo.

Fasihi ya watoto kama sanaa nyingine yoyote, ni chombo chenye misingi yake katika ubunifu. Kwa ujumla ni sanaa inayochochewa na hali halisi katika mazingira ya kijamii. Sanaa hii huweza kueleza matukio ya jamii, ikadhihirisha matumaini na matarajio yao. Fasihi huwakilisha hali, ushirikiano na mipinzano katika jamii. Inapendekeza aina mbalimbali za maadili na mitazamo inayohitajika katika jamii. Ili kuelewa kikundi fulani cha jamii, hasa utamaduni wao sharti mwanajamii arejelee fasihi yao iwe simulizi au andishi, hadithi zao za masimulizi na za maandishi, maigizo yao na mashairi. Fasihi nzuri inaweza kuchukuliwa kama kioo halisi ya jamii. Kupitia kejeli, methali na viashiria, waandishi na wasimulizi huwasilisha mawazo, fikra na hisia kuhusu matatizo ya kijamii pamoja na kuikosoa jamii hiyo. Kwa mfano, methali ni somo katika busara, ukarimu, uvumilivu na hekima yote ambayo ni muhimu katika kuwapa mwongozo wanajamii pamoja na kuleta utulivu katika jamii.

Dhima za fasihi ya watoto ni nyingi sana kutegemeana na utanzu husika, muktadha wa jamii, na kadhalika. Wataalamu wa fasihi ya watoto kutoka maeneo mbalimbali wameweza kuzibainisha dhima hizi kulingana na malengo yao tofauti. Kwa mfano, Jacobs (1961, katika Bakize- kipo mitamboni) anaelezea dhima ya fasihi ya watoto hasa kwa kujikita katika bunilizi za kihistoria za Kimarekani. Dhima hizi zaweza pia za kiulimwengu wala sio eneo la Marekani tu. Yeye anabainisha dhima zifuatazo:

1. *Bunilizi za kihistoria humpa mtoto vionjo vipya.* Zinaleta upya na ladha mpya katika chakula, mavazi, malazi, mila, burudani, na hata katika lugha. Zina maudhui yanayokata kiu: kwa mfano Safari za hatari, maajabu, maisha ya nyumbani, uhamaji na kadhalika.
2. *Kuwawezesha watoto kuiga mambo mazuri.* Bunilizi za kihistoria humfanya mtoto ajihisi na kujisikia kuwa kweli ni mtu anayeishi katika wakati mwingine tofauti na huo aliousoma katika bunilizi. Mtoto hushiriki kuishi matendo hayo katika bunilizi kupitia wahusika wanaomvutia katika kazi husika.
3. *Kuwawezesha watoto kutofautisha mambo.* Bunilizi za kihistoria za watoto huleta hali ya kuwa na mwendelezo kupitia nyakati, maana za shughuli na ujasiri wa binadamu katika utamaduni wenye maana na ule usio na maana. Baada ya mtoto kuwatambua wahusika na nafasi zao pamoja na matukio ya kihistoria, uhitaji wa mwanadamu kimaumbile, kiakili, kimihemko, kijamii, na kiroho, vyote huonesha umuhimu wake kama ilivyo leo. Hivyo, mtoto huona mwendelezo wa undugu si kwa ndugu zake tu bali hata katika hali ya ubinadamu inayomwezesha kuyaona maisha kutoka muda hadi muda, kizazi hadi kizazi.
4. *Kuwapa watoto uwezo wa kutathmini na kuamua.* Bunilizi za kihistoria ni njia nzuri pia ya kumwezesha mtoto kuuhukumu wakati uliopita, na kuwa na mwono wa leo kupitia tajriba ya jana. Humwezesha mtoto kumuona mwanadamu alivyopambana na mazingira

yake wakati uliopita na hivyo kumtathmini ni kwa jinsi gani mwanadamu huyo ameendelea.

Shaw (1968) alifanya utafiti wa mabadiliko ya maudhui huko Marekani akijikita kuangalia kipindi cha mwaka 1850-1964. Katika utafiti huo, ilibainika kuwa fasihi ya watoto ya Kimarekani ilikuwa ikibadilika katika suala la maudhui kulingana na wakati na changamoto zake. Kwa ujumla, fasihi ya watoto ilionekana kutekeleza dhima zifuatazo:

a) *Dhima ya kuadilisha.* Kazi hizi zilijumuisha ngano na simulizi za kimaadili, fasihi ya kidini, simulizi za Kibiblia, dini za kiulimwengu, watakatifu na mashujaa kwa nia ya kuleta maadili, uzalendo, sherehe za kidini.

b) *Dhima ya kushughulikia matatizo katika makuzi ya watoto.* Kazi hizi zilijumuisha kugundua majukumu au kazi yao, simulizi zinazowahusu wasichana, uhitaji wa ulinzi wa kimwili, bunilizi za kweli, simulizi zilizojikita katika vipaji, kukubalika, mahitaji ya kumilikiwa, simulizi za kifamilia, na matatizo maalumu.

c) *Dhima ya kuwasafirisha watoto sehemu mbalimbali ili kuwaelewa watu ugenini.* Kazi hizi za watoto zilijumuisha kutoa ushauri wa safari za mbali, majirani wa huko ugenini, watoto wa ugenini, maisha ya ugenini.

d) *Kuwaimarisha watoto kwa kuwasimulia maisha ya mashujaa.* Kazi za watoto ziliwapa watoto hamu ya kushinda udhaifu kwa kujumuisha watakatifu na watenda dhambi, mashujaa jeuri, ngano za mashujaa, bunilizi za kitawasifu, hekaya, visaasili na ngano, simulizi za vita, simulizi za wachunga ng'ombe na migogoro ya mipaka, simulizi za shuleni, kushinda woga.

e) *Kuwapa vichekesho na simulizi za ulaghai.* Hizi zililenga kuleta mabadiliko, fantasia ya kisasa, simulizi za ajabu, mazingaombwe, bunilizi za kufikirika, safari za kiromansia, vitabu vyenye vichekesho, kazi za kipuuzi na simulizi za likizo.

f) *Kuwapa msukumo wa kutaka kujua.*Zilijumuisha bunilizi za kihistoria, simulizi za mazoea, simulizi za kisayansi, watu na matukio ya zamani na Marekani iliyotukuka.

Naye Hunt (1999), anadai kwamba dhima ya fasihi ya watoto ni pana kwa kuwa inategemeana na mahitaji husika na kwa kipindi tofauti. Kwa mfano, akielezea dhima ya vitabu vya fasihi ya watoto, anasema kuwa:

i. Baadhi ya vitabu hivyo ni vizuri kwa kupoteza wakati,

ii. Vingine ni vizuri kwa kupata elimu,

iii. Vitabu vingine ni vizuri katika kupanua uwezo wa kufikiri,

iv. au vizuri kwa kurithisha tamaduni na maadili ya kijamii,

v. au vizuri kwa kupambana na masuala kadhaa au kupambana na matatizo mf. magonjwa, n.k.

vi. Vizuri kusoma katika namna ya usomaji ili kupata weledi wa usomaji kama ilivyo kwa utamaduni wa kazi za watu wazima,

vii. Vizuri kwa kupambana na ubaguzi.

Ngugi (2011) anabaisha kwamba fasihi ya watoto kama ilivyo ile ya watu wazima, inayo dhima muhimu sana katika jamii ya watoto na jamii pana kwa ujumla. Baadhi ya dhima hizo anazielezea vizuri kama ifuatavyo:

> ... Mojawapo ya dhima hizi ni kujiburudisha. Dhima ya pili ya kusoma ni kutaka kujiondoa katika hali fulani ya matatizo anayopitia mtoto. Usomaji wa hadithi huwapa watoto nafasi ya kujisahaulisha au kuondoka kwa muda kwenye hali ya matatizo katika maisha. Dhima hii ni muhimu sio tu kwa watoto bali hata kwa watu wazima wanaohitaji kujiliwaza na kutoka kwa muda kwenye hali ngumu za kimaisha. Wasomaji-shabiki husoma kwa sababu wanafahamu kuwa vitabu huchachawisha ubunifu. Dhima nyingine ya fasihi ya watoto ni kwamba hutusaidia kujielewa na kuwaelewa watu wengine. Mwisho, ni kwamba, watoto husoma ili waweze kupata uzoefu na kuelewa umbo la lugha. Watoto wanaweza kutambua matumizi mbalimbali ya lugha kupitia wahusika katika hadithi na baadaye kupata maarifa ya matumizi ya lugha ambayo yatamsaidia kujieleza vilivyo... (uk. 87).

Tena, Ngugi (2012) anayarudia mawazo yake ya (2011) kwa kusisitiza kwamba kama ilivyo fasihi ya watu wazima, fasihi ya watoto huwafanya watoto waburudike na kujielimisha. Anafafanua kuwa fasihi hii kuwaelimisha watoto kwa kupanua mawazo ya watoto kutokana na maisha ya watu wengine katika jamii. Kwa njia hiyo, mtoto hupata maonyo, mawaidha, makatazo na maelekezo. Vilevile, anaeleza kwamba fasihi hii huendeleza utamaduni kwa kueneza au kuwarithisha watoto mambo yanayothaminiwa na jamii ili wayaendeleze na kuyahifadhi, kama vile kudumisha mila za kijamii, na kadhalika.

Wataalamu Matundura, Kobia and Mukuthuria (2013) wanaeleza kwamba fasihi ya watoto huzua ragba kubwa miongoni mwa wanajamii kwa sababu huhusu kitengo cha jamii ambacho takribani kila mtu katika jamii ana uhusiano nacho. Dhima hiyo imekwenda mbali kidogo kwa kuonesha kwamba fasihi ya watoto pia, ina manufaa makubwa kwa watu wazima. Matundura na wenzake (2013), wanaongeza kuwa fasihi ya watoto ni suala nyeti kwa sababu fasihi hiyo hutoa mchango mkubwa katika kukuza taswira ya watoto kuhusiana na maisha yao wenyewe na ulimwengu pindi watakapokuwa watu wazima. Mwisho, wataalamu hao wanadai kuwa fasihi ya watoto huwapa watoto maarifa na ukweli kuhusu hatua ya maendeleo iliyofikiwa na jamii zao. Katika kufupisha hoja zao kuhusu dhima ya fasihi ya watoto, wanasema:

> Fasihi ya watoto ni nyenzo muhimu ya kuwasaidia watoto kuelewa mazingira ya nyumbani, jamii zao na ulimwengu kwa ujumla. Hata kabla ya watoto kujua kusoma, jamaa zao, wanaowatunza na walimu huwafundisha hadithi kuhusu watu wa sehemu nyingine ulimwenguni na wakati mwingine hadithi za zamani kuhusu watu ambao maisha yao yanafanana na yao. Ujumbe katika hadithi hizi unaweza kuhifadhiwa katika kumbukumbu za watoto hawa maisha yao yote (uk. 31).

Halikadhalika, Anderson (2013) anakiri kuwa fasihi ya watoto katika jamii inayo majukumu mengi ambayo si rahisi kuyaorodhesha yote. Hata hivyo, yeye amejaribu kuorodhesha dhima hizo za fasihi ya watoto kama ifuatavyo:

i. Kuimarisha uhusiano kati ya mtoto na watu wazima kwa kuwa humsaidia katika kusoma kazi zake hizo za kifasihi,

ii. Kujisikia raha hasa kwa kujitoma kwenye ulimwengu wa kifantasia au safari zenye mikiki,

iii. Kukuza mitazamo faafu kuhusu usomaji wa vitabu kama nyenzo muhimu ya kujitajirisha kimaarifa katika maisha yao,

iv. Huchochea makuzi au maendeleo ya urazini/uwezo wa kufikiri,

v. Huchochea na kukuza uwezo wa mtoto wa kufikiri na kubuni,

vi. Hupanua uwezo wa mtoto wa kumakinika katika mambo mbalimbali katika maisha yake ya kila siku,

vii. Humwezesha mtoto kuhisi matatizo na hisia za watu wengine,

viii. Humfunza mtoto njia mbalimbali za kukabiliana na hisia na matatizo yake,

ix. Hupanua wigo wa kufahamu ulimwengu kwa kuwa hujifunza mambo ya ulimwengu kwa shauku,

x. Humwezesha mtoto kufahamu urithi wake na wa tamaduni nyingine,

xi. Hupata maarifa mapya yanayohusiana na mazingira,

xii. Humwezesha mtoto kupata historia upya kuhusu jamii yake,

Kwa ujumla basi, fasihi ya watoto huelimisha kwa kupanua mawazo ya watoto kutokana na maisha ya watu wengine. Vilevile hutoa maonyo, mawaidha, makatazo na maelekezo. Hivyo basi fasihi ya watoto ni njia mwafaka ya kuchuja jamii ya mtoto na kuielekeza. Katika fasihi ya watoto, msanii hujaribu kujenga ulimwengu mzima ambao unafanana na maisha halisi. Kwa upande mwingine, tunaweza kupata fasihi ambayo hujenga ulimwengu wa kufikirika usiofanana na maisha halisi lakini unaoweza kukubalika. Aina hizi zote huwa na vitendo vinavyoipelekea iwe na uhalisia. Huburudisha kupitia kugusa hisia za watoto, wakafurahi na kucheka; hivyo basi kuwaletea uchangamfu katika maisha. Vilevile, fasihi huendeleza utamaduni kwa kueneza au kuwapokeza watoto mambo yanayothaminiwa na jamii ili wayaendeleze na kuyahifadhi. Uzingativu kama vile mila hudumisha jamii.

Mara nyingi imethibitishwa kuwa mwingiliano kati ya watoto na hadithi una maana kubwa kwa maendeleo ya kibinafsi na kijamii. Kwa mfano, imependekezwa kuwa mara nyingi binadamu kwa kiasi fulani huwa ni sehemu ya kile alichokisoma. Vilevile, 'hadithi tunazowaambia watoto, maelezo tunayowapa ili waweze kupata ufahamu na uzoefu wa kitamaduni, huwa kama aina ya ramani, inayowaongoza watoto katika kupata maana fulani katika ulimwengu tunamoishi. Hadithi hizi huchangia katika kuwajengea watoto utambulisho, utambulisho ambao ni wa kibinafsi na wa kijamii. Kwa namna fulani, hoja hii inaweza kuwa wazi ikichukuliwa kuwa watoto huweza tu kukua kupitia tajriba za kijamii na ulimwengu unaowazingira, na kwa kuwa hadithi ni sehemu ya ukuaji wao, basi huchangia katika harakati ya kumtamadunisha mtoto.

Ukweli ni kwamba, watoto wanaokulia, katika jamii yoyote ile hujifunza kuhusu wao ni nani na uhusiano wao na jamii hiyo ambayo wao ni sehemu yake ni upi, jinsi wanavyopaswa kufikiri na kutenda ndani ya jamii; kwa maana nyingine ni kwamba wao hujenga utambulisho ndani ya mazingira ya kijamii. Katika mchakato huu wa kujifunza na kutambua wao ni nani huwa pia wanajifunza wao si kina nani; kwa namna fulani wanatambua kuwa wao ni tofauti na watoto kutoka katika maeneo mengine ya kihistoria, kijiografia, na kijamii. Hata hivyo, katika baadhi ya hali isiyo ya kawaida, jamii hujikuta katika hali ya mivutano. Katika hali kama hizi watoto wanaweza kujifunza kuwa wao sio tu tofauti na watoto kutoka katika jamii nyingine lakini kuna mtazamo wa`sisi ' dhidi ya 'wao'. Katika hali kama hii, wanajamii wa kutoka jamii nyingine hawachukuliwi tu kuwa tofauti bali huonekana kama tishio kwa jamii husika. Jambo ambalo

linazua migogoro na mivutano katika jamii na kupelekea wanajamii wakiwemo watoto kukosa mshikamano wa kitaifa. Inapotokea hivzo, watoto wanahitaji kuelimishwa mapema kujenga utangamano wa kijamii, kitaifa na hata kieneo. Hili laweza kufanyika kupitia fasihi wanazopewa inayoonyesha umuhimu wa kuwa na utangamano katika jamii.

**Fasihi ya Watoto na Utaifa**

Kama tulivyoelezea hapo mwanzoni, fasihi kwa jumla huwa na malengo ya kuelimisha, kutoa mwanga na maadili na huweza kuchangia katika kuleta mabadiliko katika jamii. Kwa sababu hiyo fasihi ya watoto ina wajibu mkuu katika uwanja wa utamaduni wa kijamii na siasa za kijamii. Vilevile, fasihi ya watoto kupitia kwa hadithi wanazopokea huelimisha na kuathiri akili changa ya watoto ili waweze kuitikia vilivyo kwa hali mbalimbali pamoja na changamaoto wanazokumbano nazo katika jamii halisi. Changamoto hizi zinaweza kuwa za kimazingira, kisaikolojia au kiroho. Fasihi ya watoto husaidia mtu katika kutambua hulka yake kupitia kueleimisha hisia, kuchochea akili na kuiratibu kwa mujibu wa akili na roho.

Kimsingi, uamilifu wa fasihi huenda sambamba na harakati tofauti za kijamii kama vile malezi, uzalishaji mali, jando, tohara, kifo, uzazi, ukulima, ufugaji na kadhalika. Aina na uamilifu wa faaisi hasa fasihi simulizi hutegemea miktadha ya kijamii, haja ya kujieleza, udumishaji wa mafunzo, uzinagtive wa maadili pamoja na masuala ya malezi na maelekezo ya kijamii.

Fasihi ya watoto inaweza kutumika kama chombo muhimu cha kuwajamiisha watoto. Kipindi cha utotoni ni wakati ambao tabia hujengeka. Huu ndio wakati mwafaka wa kujenga wasomaji ambao watakuwa watu wa kujifunza kusoma kwa muda mrefu kwani tabia inayojengwa tangu utotoni hudumu kwa muda mrefu. Hadithi ambazo zinapandwa katika akili na fikra zao mapema, ndizo zitaunda mkondo wao wa kufikiria kuhusu wao wenyewe na ulimwengu wanamoishi. Kijumla, kipindi cha utotoni ni kipindi muhimu katika uendelezaji wa jamii yoyote ile. Ni kipindi ambacho watoto wanahitaji kufunzwa utaifa kwa dhati.Tanzu mbalimbali za fasihi ni nyenzo muhimu za kufunzia tabia miongoni mwa watoto. Watato watakua wakijua ni lipi la kufanya na lipi la kuacha kutoka na hadithi na tamathali ya misemo.

Ngugi (2012) anaeleza namna ambavyo vipengele vya utaifa vinaweza kujumuishwa katika fasihi ya watoto ili kupokezwa kwa watoto. Kwa mfano jinsi wanajeshi wanavyoonyesha ujasiri katika kulinda mipaka ya nchi ya Kenya kipindi fulani cha historia ya nchi. Pia, wanaweza kuonyeshwa hali mbalimbali ya maisha ya watu kutoka katika mataifa-finyu mbalimbali ambayo yanajenga nchi ya Kenya. Hii inaweza kuwa njia moja ya kumfanya mtoto kujenga uelewa wa tamaduni za watu wa jamii tofauti. Ni kupitia kwa fasihi ambapo msomaji wa kazi fulani hujipata kuwa amemulikwa kupitia binadamu mwingine, na akautazama ulimwengu kupitia macho ya kundi la jamii nyingine. Katika harakati hiyo ya kusoma kuhusu maisha ya watu wengine, msomaji huyo anajifunza na kutambua kuwa binadamu wengine wana mafikra na hata hisia kama zake/zao. Kwa hivyo, watoto wanahitaji kusimuliwa hadithi anuwai zinazomulika tamaduni za mataifa-finyu mbalimbali nchini. Watoto wanaweza kuganiwa hadithi zinazomulika historia moja ya nchi hasa upiganiaji wa uhuru. Vitabu vya kihistoria vinakuwa muhimu hapa katika kumbainishia mtoto harakati za ukombozi. Mwandishi wa fasihi ya watoto anaweza kuyamulika maisha ya watoto kuanzia mataifa-finyu mbalimbali na jinsi yalivyoendesha shughuli zao nyakati za enzi za ukoloni.

Jambo lingine muhimu ni kuwa; ili watoto wajione kuwa wao ni sehemu ya taifa la Kenya na ni wa Kenya halisi, ni muhimu kwanza wafahamishwe kuhusu nchi yao nje ya vitabu vya kiada. Aina hii ya ufahamisho inaweza kupatikana kupitia kusoma vitabu ambavyo vimeandikwa na

Wakenya wenyewe kuhusu Kenya. Haina maana kuzungumzia kuhusu utaifa ikiwa watoto watakuzwa kupitia fasihi ya kigeni ambayo hawajitambulishi nayo. Pili, uandishi na usomaji wa vitabu ambavyo vimeandikwa kwa lugha ya Kiswahili utasaidia kujenga hisia bora kuhusu lugha ya Kiswahili ambayo ni lugha ya taifa miongoni mwa watoto. Tukumbuke kuwa uamuzi wa Kenya kukifanya Kiswahili kuwa lugha ya taifa ulikusudia kuleta maendeleo ya nchi kwa jumla. Hivyo basi kusaidia katika ujenzi wa taifa la Kenya.

Waandishi wengi wa vitabu vya watoto nchini Kenya hawaandiki tu vitabu vya watoto kuhusu nchi ya Kenya, bali husimulia hadithi ambazo zinamulika utamaduni wa wanajamii, jinsi Wakenya wanavyoingiliana, na kutangamana, ndoto zao na imani zao. Ni muhimu kwa watoto kuonyeshwa fikra za watu wengine katika taifa zima ili waweze kuelewa tofauti na uwiano uliopo miongoni mwa watu. Jambo hili huenda likawasaidia kujaribu kujenga umoja ambao utasaidia kuboresha maisha ya Wakenya wote. Ni kweli kama wanavyodai wasomi kuwa vitabu vizuri ni 'mwanaelimu–bubu' na hufunza mengi zaidi ya yaliyomo.

Suala la malighafi ya pamoja na jinsi ya kutunza malighafi hayo ni muhimu kupokezwa kwa watoto kupitia fasihi. Watoto wanaweza kusimuliwa hadithi ambazo zinaonyesha makundi ya watoto wakitunza mazingira yao. Kwa jinsi hii, watafahamu kuwa mazingira yanapokuwa mazuri, jamii huweza kuishi vyema bila madhara yoyote. Mafunzo haya yanaweza kumsaidia mtoto kujua namna ya kuepukana na usumbufu kama vile maradhi, njaa na ukosefu wa hewa safi.

Jambo lingine kuhusu kujenga utaifa ni kwamba watoto wafunzwe maana ya wimbo wa taifa kama fasihi ya taifa. Wimbo wa taifa kama tulivyoeleza ni ishara ya kitambulisho cha taifa. Kwa hivyo, kama sehemu ya fasihi simulizi na vilevile andishi ambayo watoto hukumbana nayo mara tu wanapoingia shuleni, ni muhimu wafahamishwe maana ya maneno katika wimbo huo wa taifa mapema, isiwe ni kukariri tu kiholela kimazoea. Ni kweli kwamba baadhi ya watoto hawafahamu maana ya maneno yanayopatikana katika wimbo wa taifa na wengine huchanganya matamshi ya maneno. Kwa hivyo ni jukumu la walimu kuwafunza kwa usanifu matamshi ya kila neno na maana yake.

Watoto wanaweza kuandikiwa na kufunzwa fasihi inayohusiana na bendera ya taifa. Maana ya rangi zinazopatikana katika bendera ya taifa zinaweza kuelezewa watoto kupitia hadithi mbalimbali. Kwa mfano; umuhimu wa kujivunia rangi yetu; umwagikaji wa damu; pamoja na mbinu za kuleta amani nchini.

Kulingana na Brooks na wengine (1982), fasihi ina jukumu la kuendeleza na kuimarisha maadili ya kijamii, hisia za umoja, usawa na kuendeleza swala la kuvumiliana; kuoneana huruma, ugavi sawa wa mali, kujali, uwajibikaji na uwezo wa kusuluhisha migogoro kupitia kwa njia ambazo si za kimabavu. Hivyo basi fasihi ya watoto inaweza kuwa chombo cha kufikia malengo haya. Kupitia kwa fasihi, watoto wanaweza kufunzwa kwa njia ya kisanii kuhusu maadili ya kijamii ambayo ni ya kimsingi, (Christian Children's Fund Kenya, 2002). Maadili haya ni; wema, upendo, amani, heshima, uaminifu, uwajibikaji, furaha, uhuru, uvumilivu, ukawaida, unyenyekevu, ushirikiano na umoja.

**Hitimisho**
Hatuna budi kupigia debe harakati za kukuza ufundishaji wa fasihi ya watoto huku tukidhihirisha wazi dhima yake katika kumulika hali mbalimbali za jamii. Tunahitaji kubainisha sifa zake za kisanii na kutoa mwongozo kwa walimu kuhusu jinsi ya kukabiliana na somo hili. Sifa ya fasihi

kama chombo cha kuelimisha na kuwajamiisha watoto inahitaji kukuzwa miongoni mwa watoto wote wa shule za msingi na sekondari. Tunaamini kwamba fasihi ya watoto inaweza kutumiwa kama kivuko cha tamaduni mbalimbali zinazopatikana humu nchini na vilevile inaweza kutumika kama chombo cha kufunzia utaifa na utangamano katika jamii.

## Marejeleo

Anderson, N. A. (ed.) (2013). *Elementary Children's Literature: Infancy through Age 13*, 4th Edition. Pearson.

Bakize, L. H. (2017). *Kitangulizi cha Uga wa Fasihi ya Watoto: Nadharia na Uchambuzi.* Harare: Mswada ambao unasubiri kuchapishwa.

Christian Children's Fund. (2002). *Living Values: An Educational Program.* Nairobi: Christian Children's Fund- Kenya.

Hunt, P. (ed.). (1999). *Understanding Children's Literature: Key Essays from the International Companion Encyclopedia of Children's Literature.* New York: Routledge.

Jacobs, L. B. (1961). Historical Fiction for Children, *The Reading Teacher*, Explorations in Reading Research, Juz. 14 (3) 191-194. [Mtandaoni] inapatikana: http://www.jstor.org/stable/20197363 [2018, Julai, 6].

Matundura, E., Kobia, J., na Mukuthuria, M. (2013). "Taswira Dumifu za Uana katika Fasihi ya Kiswahili ya Watoto", katika *Mulika*, Na. 32, kur. 28-47.Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Mbatia, M. (2012). Suala la Utaifa wa Kenya: Nafasi ya Kiswahili. Katika Momanyi Clara na wengine, (Wahr). *Kiswahili na Utaifa Nchini.*Nairobi: Twaweza Communications. Kur. 3-10.

Njogu, K. (2012). "Kiswahili, Kuaminiana na Utaifa", Katika Momanyi Clara na wengine, (Wahr). *Kiswahili na Utaifa Nchini.* Nairobi: Twaweza Communications. Wah. Kimani Njogu na wengine, Kur.66-77.

Ngugi, P. M. (2011).Ufundishaji wa Fasihi ya Watoto katika Shule za Msingi Nchini Kenya, katika *Kioo cha Lugha*, Juz. 9, Kur. 84-94.Dar es Salaam: Taasisi ya Taaluma za Kiswahili.Kur. 84-94.

Ngugi, P. M. Y. (2012). "Tafsiri katika Fasihi ya Watoto", *Mulika*, 31: kur.12-26.Dar es Salaam: Taasisi ya Taaluma za Kiswahili.

Ngugi, P. M. (2012). "Mitaala ya Kiswahili katika Elimu na Utaifa: Nafasi ya Fasihi ya watoto katika Uendelezaji na Uimarishaji wa Utaifa"..Nairobi: Twaweza Communications. Kur. 106-120.

Shaw, J. D. (1968). Children's Fiction and American History, *Elementary English*, Juz. 45, Na. 1. Kur. 89-94, National Council of Teachers of English

The Constitution of Kenya Review Commission (CKRC). 2001. *Making Informed Choices: A Handbook for Civic Education.*Nairobi: Constitution and Reform Education Consortium.